





## Kilicho ndani ya Kasha


Ruta Mini



Kigawi cha Umeme Kiweko


Kiweko


#7 Skurubu za Mbao (2)


Nanga za Ukuta Mkavu (2)

## Zana Zinazopendekezwa



Keekee


Msumari wa Keekee Milimita 5.5 (inchi 7/32)


#2 Bisibisi ya Phillips


Kitia alama



Pimamaji



## 1 | **Sanidi Starlink Yako**

Anza kwa kuhakikisha Starlink yako imesanidiwa na kuunganishwa kwenye intaneti kabla ya kusanidi ruta yako.

Unganisha kwenye mtandao wako uliopo wa WiFi ya Starlink kutoka kwenye kifaa chako.





## 2 | **Weka Ruta Kwenye Nafasi Zake**

Weka ruta katika eneo unalotaka.

Tunapendekeza miongozo ifuatayo ya kusanidi mtandao wako wa wavu:
- **Kwa utendaji bora tumia muunganisho wa waya kwenda kwenye ruta yako kuu ya Starlink au Starlink Mini.**
- Usiweke ruta zaidi ya vyumba viwili mbali na kila moja.
- Epuka vizuizi vingi (mfano: kuta za saruji na vifaa vya chuma)
- Weka ruta kwenye sehemu ya juu kutoka ardhini, kama vile kwenye rafu.

Rudia kwa nodi za wavu za ziada.







## 3 | Chagua Mbinu ya Kufunga

Chagua njia unayopendelea ya kufunga, ama kwenye meza au ukutani na ufunge kiweko.

Maelezo zaidi kuhusu kufunga kiweko yatatolewa baadaye kwenye hati hii.






## 4 | Unganisha kwenye Mtandao


Ingiza kebo ya umeme nyuma ya ruta na uchomeke kigawi cha umeme kwenye soketi ya umeme. LED itawaka ikiashiria kuwa kifaa kimeunganishwa kwenye umeme.

Ruta Mini ya Starlink inaweza kuunganishwa na mfumo wako wa sasa wa Starlink (isipokuwa Ruta ya Gen 1) ama kwa waya au bila waya. Kwa muunganisho wa waya kwenda kwenye Seti ya Starlink Mini, tumia Kebo ya Ethaneti ya Starlink Mini ya mita 15. Ikiwa unaunganisha kwenye ruta nyingine ya Starlink, tumia RJ45 Cat5e au zaidi. Kwa muunganisho usiotumia waya, washa ruta yako na ufuate vidokezi kwenye programu.

Maelezo zaidi kuhusu wavu wa waya na usio wa waya yanapatikana baadaye kwenye hati.




## MWONGOZO WA WAVU WENYE WAYA



1. Sanidi Seti yako ya Starlink kama inavyoonyeshwa kwenye maelekezo ya kufunga na uhakikishe kuwa uko mtandaoni.
2. Weka Ruta Mini yako ya Starlink katika eneo unalotaka na uunganishe kigawi cha umeme.
3. Chomeka kebo ya ethaneti kwenye tundu la LAN nyuma ya ruta yako iliyopo ya Starlink au Starlink Mini. Kwa Gen 3 utahitaji kuondoa kifuniko cha kinga ili kufikia matundu.
4. Pitisha kebo ya ethaneti kutoka kwenye ruta kuu hadi kwenye Ruta Mini yako ya Starlink. Unganisha kwenye tundu la WAN la ruta yako (alama ya Starlink) ili kuunda mtandao wa wavu wenye waya.
5. Rudia kwa nodi za wavu za ziada.

## MWONGOZO WA WAVU BILA WAYA






1. Hakikisha Seti yako ya Starlink imesanidiwa na kuunganishwa kwenye intaneti kabla ya kuongeza nodi zako za wavu.
2. Pata maeneo yanayofaa ya kufunga nodi zako za wavu na uzichomeke kwenye soketi za umeme.
3. Fungua Programu ya Starlink.
4. Subiri dakika 1-2 ili arifa ya "Nodi Mpya ya (za) Wavu" ionekane kwenye programu.
5. Ikiwa arifa haionekani kwenye programu, jaribu kuweka ruta yako karibu na ruta kuu.
6. Bofya "Unganisha" au "Unganisha Zote". Nodi zitaanza kuunganishwa kwenye skrini ya "Mtandao". Muunganisho utachukua takriban dakika 1-5.
7. Rudia kwa nodi za wavu za ziada.

## KUFUNGA KIWEKO CHA RUTA

### 1 | **Tia Alama na Utoboe Mashimo ya Kiunzi**


Tumia kiunzi kama mwongozo ili kutia alama maeneo ya mashimo kisha uchimbe ukitumia keekee ya milimita 5.5 (inchi 7/32).






### 2 | **Funga Kiunzi Kwenye Sehemu**

Funga nanga za ukuta mkavu kwenye mashimo, kisha ukaze Kiunzi ukitumia skurubu ulizopewa.



### 3 | **Funga Ruta Ndani ya Kiunzi**

Chomeka ruta kwenye kiweko kilichofungwa ukutani kwa uangalifu, ukihakikisha kifaa hicho kimeingia sawasawa baada ya kufungwa kikamilifu.

